

CHANJO

Pata chanjo zako ili uendelee kuwa na afya njema

Chanjo ni sindano unazodungwa ili uepuke kuwa mgonjwa


JE KWA NINI NINAHITAJI CHANJO?

Nchini Marekani, magonjwa mengi ambayo yaliwahi kuwafanya watu wawe wagonjwa zaidi yanatokomea. Mojawapo ya sababu kuu ya magonjwa haya kutokomea ni matumizi ya chanjo. Chanjo husaidia kuzuia magonjwa yanayoweza kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Ukidungwa sindano unazohitaji, unajikinga pamoja na wapendwa wako dhidi ya magonjwa.

CHANJO ZINAFANYA KAZI KIVIPI?

Chanjo inatengenezwa kutoka kwenye virusi vile vile (pia huitwa viini) vinavyosababisha ugonjwa. Viini vinavyotumika kutengeneza chanjo huwa "vimekufa" au dhaifu. Havitakufanya kuwa mgonjwa. Badala yake, vitasaidia mwili wako kupigana na viini na magonjwa yanayosababishwa na viini vile.

NI NANI ANAYEHITAJI CHANJO?



KUNAZO ATHARI ZA KANDO?

Watu wengine huwa na athari ndogo za kando baada ya kuchanjwa. Hizi zinapaswa kutoweka baada ya siku moja au mbili.




Maumivu/Wekundu

Upele Mdogo

Homa Ndogo

Watu wengine huwa na athari sugu za kando zisizo za kawaida, baada ya kuchanjwa. Mara nyingi, athari hizi hutokea dakika chache au saa chache baada ya kuchanjwa.



Tatizo la Kupumua

Kuhisi Kizunguzungu

Upele/Mwasho

Uvimbe wa Koo

NINAHITAJI CHANJO ZIPI?

Jedwali lililo upande ule mwingine linaonyesha chanjo ambazo watu wazima na watoto wanahitaji. Watu wazima ambao hawakupata chanjo zote walipokuwa watoto huenda wahitaji chanjo nyingi zaidi. Zungumza na daktari wako ili ujue ni chanjo zipi unazohitaji

Kwa maelezo zaidi, nenda kwenye: www.vaccines.gov

Jina la daktari wangu:

Nambari ya simu ya daktari wangu:

Pata chanjo zako ili uendelee kuwa na afya njema

Mwone daktari wako kwa ukaguzi wako na upate chanjo zozote mpya unazohitaji.

Chanjo zilizotiwa alama hapa chini zinahitajika kwa: _____ (Jina) _____ (Umri)

Ziara yako ijayo ni: _____ (Tarehe) _____ (Saa) _____ (asubuhi/mchana) _____ (Tarehe ya Kuzaliwa)

Inaitwaje?	Who needs it?			Chanjo ile inasaidia kuinga ugonjwa gani?	Ugonjwa ule unasababisha nini?
	Watoto* Pekee	Watoto na Watu Wazima	Watu Wazima Pekee		
<input type="checkbox"/> DTaP au Td/Tdap		X		Dondakoo	Homa, maumivu kwenye koo, kujihisi mnyonge; zinaweza kusababisha uharibifu kwenye moyo na neva
				Pepopunda	Homa, shingo kuwa ngumu, matatizo ya kumeza; zinaweza kusababisha matatizo ya kupumua
				Kifaduro	Kikohozi kibaya, mafua, kusita kwa mtoto kupumua; zinaweza kusababisha maambukizi kwenye mapafu
<input type="checkbox"/> Mafua		X		Mafua	Homa, maumivu kwenye koo, kikohozi, maumivu ya misuli; zinaweza kusababisha maambukizi kwenye mapafu
<input type="checkbox"/> HepA		X		Homa ya Manjano A	Kujihisi mchovu, macho na ngozi ya manjano; zinaweza kusababisha magonjwa ya ini, figo na damu
<input type="checkbox"/> HepB		X		Homa ya Manjano B	Kujihisi mnyonge, macho na ngozi ya manjano; zinaweza kusababisha uharibifu wa ini
<input type="checkbox"/> Hib		X		Influenza ya haemofilasi aina ya b	Zinaweza kusababisha maambukizi ya mapafu na ulaini kwenye ubongo na uti wa mgongo
<input type="checkbox"/> HPV		X		Maambukizi ya Human papillomavirus	Madutu ya sehemu nyeti; inaweza kusababisha aina tofauti za saratani
<input type="checkbox"/> IPV	X			Ugonjwa wa kupooza	Maumivu kwenye koo na maumivu ya kichwa; zinaweza kusababisha mwili kutoweza kusonga
<input type="checkbox"/> MenACWY au MenB		X		Ugonjwa wa Human papillomavirus	Homa ya ghafula na shingo kuwa ngumu; inaweza kusababisha maambukizi ya ulaini kwenye ubongo na uti wa mgongo
<input type="checkbox"/> MMR		X		Ukambi	Homa, vipele, mafua, kikohozi na macho mekundu; zinaweza kusababisha maambukizi ya mapafu
				Matumbwitumbwi	Homa, maumivu ya kichwa na uvimbe wa tezi zinazounda mate; zinaweza kusababisha maambukizi ya ulaini kwenye ubongo na uti wa mgongo
				Surua	Homa, uvimbe wa tezi, na upele
<input type="checkbox"/> PCV13 au PPSV23		X		Ugonjwa wa Pneumococcal	Maambukizi ya mapafu; unaweza kusababisha maambukizi ya damu
<input type="checkbox"/> RV1 au RV5		X		Homa ya matumbo	Homa, kutapika na kuendesha
<input type="checkbox"/> Varicella	X			Tetekuwanga	Homa na vipele vinavyowasha
<input type="checkbox"/> Zoster			X	Vipele	Upele wenye maumivu makali na malengenge

* Watoto wa miaka 0 hadi 18

Jiweke na wapendwa wako salama kiafya. Pata chanjo zako.